Makutano ya Padre Simeon Lourdel misionari wa kwanza P. Georges Paquet na Watemi (Tanzania)

Miaka mia moja kabla nije kuishi katika nchi hii – tarehe 5 februari 1871, Henri M. Stanley alifika Bagamoyo kwa watawa Wafaransa, waliokuja kutoka kisiwa cha La Réunion. Aliandika katika kitabu « jinsi nilivyokutana na Livingston » : « wana wanafunzi mazuri, nashangaa kusikia vijana hawa wakiimba nyimbo ya fahari na ushindi ya Ufaransa kama vijana wa Faubourg Saint Antoine (Paris)… »

Stanley alifika Tabora mwisho wa juni …P. Lourdel alifuata njia ile ile. Alianza msafara wake Bagamoyo, tarehe 9 jun 1878 pamoja na « Jean baptiste, mfasiri wetu » (soma katika gazeti ya W.F. no 29, januari 1879, uk. 44). P. Lourdel aliweza kuongea vizuri kiswahili alipofika Tabora, tarehe1oktoba.

Mimi, septemba 1971, nilikuja Kipalapala (Tabora) kujifunza kiswahili kwa muda wa miezi sita na baadaye nilienda Sikonge kukaa katika ploti tuliopewa na Mtemi Lugusha Mhalule, baba wa Mtemi wa mwisho – na nilifanya kazi huko tangu mwaka 1972 mpaka 1976. Mwezi wa septemba 1976, nilihamia katika wilaya ya Igunga mpaka 1984. Huko nilizianzisha kikundi changu cha ngoma pamoja na wananchi waumini wa dini mbali mbali – pamoja na walingi wangu tuliweza kushinda katika mashindano yote kwa mahusiano mwema bila ya kutumia mazingaombwe.

Tangu septemba 1988 mpaka mwisho wa mwaka 1998, nilikuwa Iboja-mishinzi (maana yake sehemu walivyoweka vichwa vya maadui juu ya ukuta wa ngome) katika nchi ya Ukune. Hapa pamoja na Mkristu mmoja, John Kazindo, mlingi na mganga wa kienyeji tukawa tena na kikindi cha ngoma ya ushindi kila mara …

Ni hapa Iboja alipofariki Mtemi Mirambo aliyekuwa amekuja kujaribu kuingia katika ngome ya Mtemi Kapela, mjomba wake. P. Lourdel alifika, Mtemi alishafariki. Tutasimulia badaye.. Hapa Iboja, nilikutana na Mtemi wa mwisho, Ndwikwa II Kapela. Aliyekuwa katika kijiji cha Kisuke peke yake pamoja na ngoma zake na ndugu mmoja wa kumpikia chakula. Alinieleza kwa kirefu juu ya maisha na vita vya Watemi wa nchi yake. Alinionyesha mkuki wa ajabu na pembe ya dawa ya Mtemi Kapela na tulienda pamoja mpaka Iwe Lya Shinga kuona sehemu aliyekuwa akikaa P. Lourdel, tangu terehe 15 aprili 1884 mpaka tarehe 15 aprili 1885(wakati wazungu wakikutana huko Berlin kugawa mapande bara la Africa!); Mwenye kiti wa kijiji cha Ngokolo, bado alikuwa akija kufanya matambiko juu ya kaburi la mama wa Mtemi Mirambo.Alinieleza pia maelezo juu yu nyumba ya P. Lourdel.

Pamoja na marafiki wa Iboja, niliandika historia ya Watemi wa Ukune baada ya ubatizo wa Mtemi Georges Ndwikwa. Yeye alikuwa pamoja nami katika sikukuu zote za Iboja, hasa wakati wa Pasaka alikuwa na kivaa nguo zake za kitemi pamoja na ngozi ya simba kichwani. Tulikuwa pamoja na ngoma kama alivyoandikwa zamani P. Lourdel katika barua ya tarehe 2 juni 1879 : “ kwa Wanyamwezi, ngoma ina shabaha ya pekee : inatangaza maadui wanapofika, inaita askari kujiandaa kwa vita, na mwisho ya vita inawashangilia askari kwa kuwashambulia maadui – hakuna sikukuu au kilio bila ngoma…”

Tutafuata sasa maadishi ya ukumbusho walioniachia, Mtemi Lugusha, P. Lourdel na Mtemi Ndwikwa.Tutaona kwamba wanaotofautiana lakini inafaa kuwasikiliza wote. Mtemi

Ndwikwa aliamini kwamba mama Subi alitumia sumu na mambo ya uchawi kumuua Mtemi Mirambo, lakini P. Lourdel na Mtemi Lugusha walifikiri kwamba alikufa kwa ugonjwa tu. Inafaa kuyalinda yote tuwe na kumbukumbu ya kuwafanya watu wenye tamaduni tofauti waweze kuwa pamoja na kusikilizana. Nami nilifurahi kukutana hapo Paris na Raïs Julius Nyerere na Baadaye Raïs Jakaya Kikwete.

Chimbuko La Utemi zamani milele za kale.

Watu watatu, wawili wazima, mmoja kipofu hana macho, wakaenda maporini kutembea… Wa kwanza akaenda, akaokota n'gombe, wa pili akaenda, akaokota mbuzi na kondoo. Walipokutana, moja akasema : « mimi nimeokota ng'ombe hawa. » wa pili akasema : « na mimi nimeokota mbuzi na kondoo.» Basi, wakashauriana, wakasema, tumwite na mwenzetu, hana macho. Tumweleze shauri la kuokota ng'ombe, mbuzi na kondoo.Basi wakamwita. Yule kipofu, hana macho alipofika mbele za watu hawa, wakampa kiti, akakaa na kawaambia ; wa kwanza : « mimi nimeokota ng'ombe. » wa pili akasema : « na mimi nimeokota mbuzi na kondoo. » Basi yule kipofu akainama na kufikiri moyoni mwake, alipoinuka akasema : « na mimi nimeokota nchi na kila kitu kilichomo inchini ni mali yangu » Basi watu wale walipimgia makofi, akawa Mtemi. Siku moja mwenye ng'ombe alilisha shamba la mwenye mbuzi, shauri likapelekwa kwa Mtemi.Kipofu akakata shauri. Mkosaji akahukumiwa alipe ng'ombe jike kwa ushahidi wa watoto wa kipofu kuona ng'ombe ilivyo kimo chake. Basi ndiyo chimbuko la Utemi hapa duniani. Mwisho.



Mtemi Lugusha Mhalule na Padre Georges Paquet (1974)

Kitabu hiki nimeandika mimi. Nimeanza leo, tarehe 21.08.1965, cha ukumbusho wa utawala wa nchi yetu kizazi cha : 1- Unyangwila / Wanyangwila ; 2 – Nguru Sikonge ; 3-Unyanyenbe,Ukimbu Wakimbu Tabora
Mwandishi wa Kitabu hiki: Lugusha Mhalule, 21 Augusti 1965.
Nimekiandika ni ukumbusho wa baadaye watu wasisahau vizazi vyetu.
Vita vya Mtemi Mkwaba wa Iringa na Wajeremani ni mwaka wa 1898.
Mtemi wa kwanza kutawala katika nchi ya Unyangwila ni Mtemi Magawa bin Igulwibi
Alizaa watoto: 1 – Luenga bin Magawa, 2 – Maleba bin Magawa, 3 – Mputa bin Magawa
4 – Mwenda bin Magawa.
Mtemi Magawa kabla hajafa aligawa watoto wake inchini: Mputa bin Magawa akapewa nchi ya Ngulu Sikonge kutawala; Mwenda bin Magawa akapewa nchi ya Unyanyembe kutawala;

Maleba bin Magawa huyu alibaki ya Unyangwila na ndiye aliletawala Unyangwila baada ya mauti ya baba yake Magawa Igulwibi.

1 - Mtemi Mputa bin Magawa ndiye wa kwanza kutawala katika nchi ya Nguru Sikonge.
Mtemi Mputa alizaa watoto: Lusesambambi bin Mputa; Madeleka bin Mputa; Makanyansa bin Mputa. Mtemi Mputa akafa kwa ugonjwa tu.
2 –Mtemi Madeleka bin Mputa akatawala baada ya baba yake Mputa.
Amezaa watoto: Lulenga Madeleka; Pemba Moto Madeleka; Magilibanya Madeleka.
Mtemi Madeleka akafia Ugogo pamoja na ndugu yake Mtemi Lyoba wa Ugalla kwa vita vya Wagogo.
3 – Mtemi Pemba Moto Madeleka akatawala baada ya baba yake Madeleka
Nae alizaa watoto wawili: Kanyanka Pembe Moto; Malingo Pemba Moto
Mtemi Pemba Moto akafa kwa njaa, maana nchi yake ilipatwa bahati mbaya ya njaa na hataki kula chakula kutoka nchi nyingine, maana nchi kinakotoka chakula kinatoka kwa wenye kujipaka mafuta ya kufuatwa na vidudu nzii.
4 – Mtemi Malingo bin Pemba Moto akatawala baada ya baba yake Pemba Moto
Nae alizaa watoto: Kimwaga Malingo; Lukorongo Malingo
Mtemi Malingo akafa kwa ugonjwa tu.
5 - Mtemi Magilibanya Madeleka akatawala baada ya Mtemi Malingo.
Amezaa watoto: Masanja Makanyansa (Magilibanya) ; Kitindi binti Makanyansa
Mtemi Magilbanya akafa kwa ugonjwa tu.
6 - Mtemi Lukorongo Malingo wa Nhundi akatawala baada ya Mtemi Magilibanya
Alizaa watoto: Nkumba Mkilile Lukorongo; Tomazi Lukorongo.
Mtemi Lukorongo akafa kwa ugonjwa tu.
7 –Mtemi Nkumba Mkilile bin Lukorongo akatawala baada ya baba yake Lukorongo hapo Nhundi. Yeye kwa bahati mbaya hakuzaa na alikimbia vita ya Wangoni.Akakimbilia Ikonongo mpaka Ugalla; vita ilipokwisha nyuma yake, wanyikuru, yaani watumwa wake, wakamchagua mwenzao wakamtwalisha akaitwa Nkumba Mwasi, yaani Nkumba Mtumwa.
8 – Mtemi Nkumba Mwasi akatawala baada ya bwana wake Nkumba Mkilile.
Mtemi Nkumba Mkilile vita ilipokwiha akapata habari ya kama mtumwa wako Mkumba Mwasi ametawala baada yako.
9 – Mtemi Nkumba Mkilile bin Lukorongo akarudi tena kufukuza mtumwa wake yaani mnyikuru mtumwa.Mtemi Nkumba Mwasi akatolewa katika utemi; akatawala tenaNkumba Mkilile mara ya pili. Baadaye akafa na hakuzaa.
10 – Mtemi Kimwaga bin Malingo akatawala ikulu wake Mbalagani, baada ya Mtemi Nkumba Mkilile.
Kimwaga akazaa watoto: Lukawa Kimwaga; Nsehele Kimwaga; Kisali binti Kimwaga; Masanja Kimwaga; Kitindi binti Kimwaga; Lusomeno binti Kimwaga.
Mtemi Kimwaga, huyu mtoto wake Lukawa Kimwaga alikuwa mtu mwenye majivuno sana hapendi kuzugumza na watu, wala hapendi kula chakula na mtu yeyote. Basi baba yake Mtemi Kimwaga akamlani, akasema: “wewe, si mtu mwema, nikifa huwezi kurithi kiti changu cha utemi ila atawale Mhalule bin Mazwazwa, mtoto wa kaka yangu.”
Basi Mtemi Kimwaga akafa na ugonjwa tu.
11 – Mtemi Mhalule Mazwazwa wa Igombe akatawala baada ya baba yake mdogo Mtemi Kimwaga Lulenga.
Mtemi Mhalule alizaa watoto : Mawinza binti Mhalule, wajukuu wa Mazwazwa ; Mayunga Mhalule, wajukuu wa Mazwazwa ; Mbalu Kitindi binti Mhalule, wajukuu wa Mzwazwa ; Kisali binti Mhalule, wajukuu wa M. ; Kasanda binti M., wajukuu wa M. ; Maswazwa bin M., mjukuu wa M. ; Kanyanka bin M. wajukuu wa M. ; Nkombi binti M., wajukuu wa M. ;

Nyanso … ; Lugusha … ; Tamazi … ; Ishila binti …. Mtemi Mhalule alikamatwa na Wadachi, yaani Wajeremani kwa fitina ya mtu wao wa kazi ya posta Mazyala bin Lwengele , akipeleka posta Tabora na Manyoni, kilimatinde Ugogo. Siku moja, mtu wa posta, huyu Mazyala akanyanganya posta kwa nguvu na wadumuzi katika mapori ya nchi ya Mtemi Mhalule Nguru. Mtu wa posta Mazyala, akakimbia mpaka bomani Tabora kutoa riporti serekalini, kama posta nimenyanganywa na watu wa Mhalule. Basi akaondoka Mzungu Mgeremani, anaitwa Bwana Ghanza na akaja kumkamata Mtemi Mhalule, kumpeleka bomani Tabora na kuenda kwenye rumande. Serekali ikapeleleza shauri hii, hata wakapatikana watu waliomnyanganya posta Mazyala ikawa ni mtu wa Urambo kwa Mtemi Zinambaya. Watu hawa wakafungwa gerezani muda wa miaka mitano na kupigwa viboko, 25siku ya kufungwa na 25 siku ya kufunguliwa. Na ndipo Mtemi Mhalule akaachiliwa akawa huru na kuambiwa na serekali ya kama mchtaki Mtemi Zinambaya amekuponza yeye, umepata adhabu hii na masumbuko mengi kuzaniwa ya kama watu wako wanenyanganya posta ya serekali, kumbe hapana.Mtemi mhalule akakataa kumstaki Zinambaya. Basi aliporudi nyumbani kwake Igombe akapata ugonjwa na akafa 1894 na ilidhaniwa na watu ya kama kipigo na kunyanganywa mateke, na mateke ya bunduki aliyekuwa akipigwa na askari wa kigeremani, ndicho kimeleta ugonjwa wa Mtemi Mhalule Mazwazwa.Akafa. Mtemi Mhalule alikuwa na nduguze: Ilema Mazwazwa; Mpagama Mazwazwa; Mtindwa binti M.

12 –Mtemi Mayungo akatawala badala ya baba yake Mhalule.Mtemi Mayungo amekaa mwaka mmoja tu akaugua ugonjwa wa ndui, akafa.Na kabla alikuwa hajaanza kuzaa watoto.

13 –Mtemi Mbaru au Kitindi Mhalule akatawala baadala ya kaka yake Maswazwa. Mtemi Kitindi amekaa muda ya miaka mitatu tu katika kiti cha utemi; akapewa mimba yaani himila na Shabani bin Feruzi, Msumbwa wa Tabora mjini. Wakati wa kuzaa akaanza vizuri lakini basi ule mfuko wa motto ukakataa kutoka, ikawa ndio sababu ya Mtem Kitindi afariki na motto wake akafa vile vile.
14 – Mtemi Kulwa bin Kidaso akatawala badala ya Mtemi Kitindi. Mtemi Kulwa Kidaso ni mtoto wa Lusomano binti Kimwaga (Mtemi No 10). Mtemi Kitindi na Kulwa Kidaso ni mtu na binamu yake. Mtemi Kulwa alitawalishwa na wanyikuru. Wanangwa, wizukulu na wagawe walikuwa hawapendi Kulwa kutawala, ila wao walikuwa wamempenda atawale Kimwaga bin Kasenya – ni mtoto wa Lusomano binti Kimwaga vile vile. Kimwaga na Mtemi Kulwa Kidaso ni mtu na kaka yake. Ni watoto wa mkwilima. Ngulu Sikonge ni kukeni kwao. Ugomvi wa wanyakuru, wanangwa, wizukulu na wagawe; Ugomvi wao ulizidi sana hata wanangwa, wizukulu na wagawe pamoja na Kimwaga Kasenya wakaenda kushitaki mbele ya serekali bomani Tabora - kuwashitaki wanyankuru wa Igombe, kwa kutawalisha Mtemi kulwa Kidaso peke yao bila mapatano na wakuu wa nchi. Shauri lilipofikishwa mbele ya serekali ya Wajeremani, wakasemezana muda wa siku tatu, halafu serekali ikawaambia: “shauri lenu. Kwanza nendeni mkasemezane kwa undugu na Mtemi Kalunde binti Ifuma Gumata wa Itetemia, Unyanyembe”. Basi wakaende kusemezana undugu wao na vile vile hawakusikilizana. Mtemi Kulwa Kidaso hakukubali na kupendezwa kumupa utemi kaka yake Kimwaga, maana baraza la undugu kikaamua kama Mtemi Kulwa bin Kidaso aache utemi na kumwachia kaka yake Kimwaga bin Kasenya. Kulwa alikataa na kusema afadhali utemi nimwadhie binamu yangu, watoto wa mjomba Mtemi Mhalule bin Mazwazwa wa No 11 . Shauri likarudishwa tena bomani Tabora; kufika kule shauri likasimama. Serekali ya Kidachi ikauliza: “ wapi watoto wa Mhalule”. Ndiyo wakasimamishwa: 1. Kanyanka Mhalule,
2. Lugusha Mhalule. Wadachi walipowatazama watoto hawa, wakamchagua Kanyanka Mhalule, huyu awe Mtemi wa Nguru Sikonge.Basi Mtemi Kulwa Kidaso akatolewa utemi.
15 –Mtemi Kanyanka Mhalule akatawala mwaka 1905. Mtemi Kanyanka alikaa katika utemi kwa muda wa miaka saba.Kabla hajafa alizaa mtoto. Wakati amezaa alikuwepo bwana shauri

wa Kidachi aitwaye Bwana Zigilli, basi Mzungu huyu akamwambia Mtemi ya kama mtoto wake huyu nimempa jina langu Zigilli bin Kanyanka. Zigilli alikufa kabla ya baba yake Kanyanka na baadaye Mtemi Kanyanka Mhalule akafa vile vile kwa ugonjwa wa kifua kikuu.
.
16 – Mtemi Mpagama bin Mazwazwa aliposikia mtoto wa kaka yake Mtemi Kanyanka Mhalule amekufa, akaja kwa ukali sana kusema mbele ya wizukulu, wanangwa,wagawe na wanyikulu ya kuwa watoto wangu wamekufa sana safari hii, mimi sitaki kuwatawalisha watoto wa Mhalule - asema (mikononi anashika mikuki) "leo tutauwana kabisa" . Wizukulu, wanangwa, wagawe na wanyikuru wakafanya mashauri na wakasikilizana ya kuwa inafaa yeye Mpagama Mazwazwa akamatwe, awe Mtemi na ndipo akaviziwa kwa maneno matamu sana kukamatwa – ndiyo akawa Mtemi mwaka wa 1910.
Mtemi Mpagama alizaa watoto: Nasoro bin M.; Kapiga bin M.; Kalunde binti M.; Kapemba binti M.; Isamba binti M. – Mtemi Mpagama alikosa na akahukumiwa kifungo cha miaka kumi kwa makosa idhini ya kuua watu wawili, na muuaji mtu anaitwa Maula wa kule Nyahua stationi, wakati wa vita kuu ya 1916. Kifungo amefungwa wakati wa enzi ya utawala wa Mwingereza na alipofunguliwa akaletwa Itetemia, Unyanyembe. Kabla hajachukuliwa kupelekwa Sikonge, hapo Itetemia, alichimba dawa mti mgando - mgimbila akakaanga na njugu mawe, akawa anaubabua mzizi wa mgimbila motoni na kutafuna pamoja na njugu, anakula na kumeza kusudi aende choo vizuri. Basi choo hakuende ila tumbo lilivimba na akafa 1923.

17 – Mtemi Kimwaga bin Masenya, 1917 akatawala baadala Mtemi Mpagama, mjomba wa Kimwaga. Kimwaga ndiye aliyeleta fitina kwa mjombaye Mpagama. Ilikuwa hivi, yule mwuuaji wa watu wawili, anaitwa Maula, alipoua, akaleta fedha sh 20/ kwa Mtemi Mpagama, kwa desturi ya zamani, maana alimwaga damu katika nchi kwa kuwaua watu hawa.Mtemi Mpagama alikataa kuzichukua fedha hizo. "Pesa hizi nikizipokea na kuzila nitakuwa muuaji mbele ya serekali". Basi wakati ule: Mzee Lela liwali wa Mtemi Mpagama, upo; Kimwaga Kasenya, upo; Lugosha Mhalule, upo na Mtemi mwenyewe Mpagama. Basi Kimwaga akasema : " Hapo tupo sisi watoto wako, mimi na Lugusha Mhalule na huyu Mzee Lela ni liwali wako, nani basi atakwenda kusema mbele ya serekali".

Mwisho Mtemi Mpagama akachukua fedha hizo Mtu mfitina, Kimwaga Kasenya, usiku akaenda bomani Sikonge (alikuwepo Bwana shauri wakati wa vita 1904). Kimwaga akamfunguza Kapulo Nasoro na kumwambia ya kama Mtemi Mpagama ameua na amekwisha kupewa sh 20/ za rushwa kwa kuua watu wawili, kule Nyasha stationi, na muaji Maula, leo hii amekwenda kula gunguli Uliwansimba. Basi Kapulo Nasoro na Kimwaga wakaenda wafungusa Bwana shauri na kumpa habari hii. Usiku ule ule, wakatuma askari kwenda kukamata Maula kule Uliwansimba na asubuhi akaenda askari kumkamata Mtemi Mpagama. Ikawa shauri kubwa ndiyo Mtemi Mpagama kupelekwa bomani Tabora, ndiyo sababu ya kufungwa miaka kumi gerezani, kwa ufitina na Kimwaga kusudi naye apate utemi; ndipo naye akatawala mwaka 1919. Naye akawa si mtu mwema mbele ya watoto na wajombaye Mtemi Mhalule Mazwazwa (No 11) - hata kwa Watemi wenziwe na hata na wanangwa wa magunguli na kila raia pia.Ndiyo akatolewa kiti cha utemi 1922.

18 – **Mtemi Lugusha bin Mhalule**, amezaliwa 1890 , na katawala bada ya Kimwaga Kasenya Lugusha ametawala tarehe 6.2.1922. Alikuwa Kigoma kwa kazi na ndiko ilikwenda kuchukuliwa na kuja kupewa kazi ya utemi. Yeye kwanza alikataa kutawala kwa kumwogopa binamu yake Mtemi Kimwaga kudhani atamroga afe. Bwana shauri alimpa barua kwenda Utetemia, Unyanyembe, kwa Mtemi Saidi Fundikira. Basi Mtemi alimwitia wazee wakuu: Mgawe Mayega wa Lurangulu; Mumero wa Isenga - akawaambia : "Mwimbieni mtoto huyu

nyimbo , Lugusha Mhalule ati anakataa kuenda kutawala Nguru Sikonge ". Mayenga Mamelo wakanimbia nyimbo na kuniambia maneno magumu sana, kusema: "nenda utawale kesho ufe, ashike mwenzio kiti ". Mwisho nikawa nalia sana, baadaye nikakubali. Mtemi Saidi Fundikira akaandika barua kumpelekea Bwana shauri , kusema : "Lugusha sasa amekubali kuenda kutawala"; na ndilo akaondoka na Wazungu 4 na askari polici 16 na wa K.A.R. 16 ya ni keya jumla askari 32.Wazungu walikuwa na wasi wasi na Kimwaga maana mtu wa matata , labda anaweza kuleta ugomvi wakati hule apigwe risasi na akufanya taabu akatolewa ndiyo kutawala kwangu.

Mimi nimezaa watoto: Mhalule Lugusha 1917 ; Mhalule Lugusha,1924; Msablia Lugusha 12.09.1920; Midelemo binti Lugusha, 3O.10.32 ; Lukorongo Lugusha,7.9.35 ; Kidaso L. 16.3.39; Mtidwa binti L. 21.4.40; Masungo binti L. 22.4.42; Lusomano binti L. 5.7.60; Useni L. 29.5.62; Mpagama L. 8.4.64……

19 – Mtoto wangu Aruni Msabila Lugusha ametawala 12.6.1941 baadala yangu, naye amezaa watoto, yaani wajukuu wa Lugusha: Maswazwa bin M. 15.11.37; Lugusha 8.5.39; Kanyanga 3.10.43; Kimwaga 31.12.46; Mawinza binti M.; Mganzo binti M. 16.2.51; Nyanzo binti M. 12.11.53; Abdala; Fundikira; Moja; Manyanda; Masumbuko au kuangahika hoi 12.5.64. Basi nchi yetu ya Tanganika ilipopata uhuru wetu mwaka 1962, ukawa mabadiliko makubwa sana. Utemi ukavunjwa – basi yake ikawa ni utemi wa jadi hauna kazi kupata mshahara. Mtoto wangu Mtemi A. Msabila Lugusha akaenda Dar es Salaam kufanya kazi ya kompani. Mwaka 1964, askari wa jeshi wa Dar es Salaam waligoma kutaka kupindua serekali na hawakuweza kwa sababu Mheshimiwa wetu Mwalimu Julius Nyerere alipiga simu, ikaenda Uengeleza kusudi aje asaidiwe. Kwa taabu hii ya askari wa jeshi, Waengeleza walituma jeshi lao kwa haraka iwezekanavyo. Jeshi hilo likaja kwa kamata wale askari wa jeshi la Dar es Salaam. Waligoma, wakakamatwa haswa koloni, basi ukawa msukosuko watu wengi wanakamatwa kuzaniwa, labda hawa ni wachochezi na wale askari waliogoma. Watu wengi sana wakakamatwa na 26.1.64, Mtoto wangu A. Msabila Lugusha naye alikamatwa na kutiwa nguvuni awawekwa kisimbani, wengine wengi wametolewa … na yeye sasa 19.7.66 ametolewa kizuizini gereza la Kiomboi, Ilamba ; amefika Sikonge 20.7.66.

Mimi Mtemi, usia wangu Lugusha Mhalule: tangu leo,15.1.68, nafahamisha watoto wangu wote na wajukuu wangu wote wakae hali ya kujua na wasije wapitiwe maneno ya kinyume na watu wajanja, wapendao kujitia katika ukoo usipokuwa wao, na ujipendekeza kuwa wao ni ukoo wa utawala wa Sikonge Nguru. Mtu huyu eti anasema kizazi kinatokea kwa Mtemi Kimwaga Lulenga, kaka yake ya Maszaswa Lulenga wa Ikulu Mbaragani, karibu na Igombe nilikozaliwa mimi; basi, mtu huyu ni mwongo sana, ujanja wake tu kutaka naye hajatawale au ukoo wake uje utawale katika nchi hii ya Sikonge Nguru.

Mtu mjanja ninayesema ni huyu Alimasi bin Kidumla si ndugu yetu awezaye kutawala katika nchi hii ya Sikonge Nguru, si Mnyangwila, si Mnyanyembe, si Mnyanguru, si wa Kigwa wala si wa Kipili hata Kisalusalu (Nguru).

Kidumla bin Mkopi ameletwa nchi ya Nguru na Mtemi Mhalule bin Mazwazwa alikuwa ni mganga tu wa madawa yake yalipendezwa na Wanyanguru na ndipo alipewa gunguli Isenegezwa karibu na Nyahua station, upande wa kaskazini, basi msije mkadanganywa na

Almasi Kidumla kusema ukoo watokea kwa Mtemi Kimwaga kama nilivyoeleza – kwanza ni uongo mtupu.

Ukoo wetu wote ni Wanyankuru kuntu. Sijasikia mtu mmoja amezaa mtoto akampa jina Mkopi au Kidumla, hapana maana yake inajulikana si ukoo.

Nawafahamisha mjue na mfahamu sana kabisa ukoo wenu hasa Wanyangwila, Wanyankuru wawezao kutawala nchi yenu ya Ngulu Sikonge, ni matumbo haya:
1. Tumbo la Mtemi Kimwaga Lulenga wa Mbalagani Igombe Nguru, mtoto wake Mkubwa Lukawa Kimwaga na mtoto wa Lukawa, a) Ntuga Lukawa, b) Nwala Lukawa na siwezi kuandika wote kizazi chao kinaendelea na kinajulikana vile vile.
2 . Tumbo letu la Mazwazwa Lulenga undugu wa Kimwaga Lulenga, tumbo moja baba na mama. Ndiyo Mazwazwa alimzaa Mtemi Mhalule Mazwazwa, Mpagama Mazwzawa, siwezi kuandika wote tumbo lao, lajulikana tu.
3 . Tumbo la mwizukulu Makibya, naye alimzaa mtoto Makinda Makibya wa gunguli inalala Nguru, nao ukoo wao unajulikana tu.
4 . Tumbo la Ndulika na mwipaye mwizukulu Msongo na watoto …
5 . Tumbo la waizukulu Kasema na kidogo wa Uliwasimba …
6 . Tumbo la mwizukulu Igula Kanyamusenga.
7 . Tumbo la mwizukulu mwana Ndenge ….
Basi haya matumbo ya Wanyankuru yawezayo kutawala vizazi katika nchi ya Sikonge Nguru.

Wasiya wa nchi ya umbo Busagali.
1 . Mwanza wa Mtemi Mtelya au Milambo Kasanda – Jina la Milambo alipewa na fundi wake Kisimba Magombo. Mtemi Milambo amekufa kwa ugonjwa tu naya amefiwa Ukune kwa mjombae.
2 . Baada ya kugabangoma Milambo badala yake akatawala Mtemi Kashindye au Mpenda Shalo Kasanda. Mpenda Shalo amekufa kwa vita vya Wangoni.
3 . Anatawala Sibuga au Katuga Milambo na baada ya Mtemi Katuga alikwenda kuwinda nyama porini, na wakati wa kurudi nyumbani, akawaona wagoli yaani wake zake wanatokea nje ya mji wanakimbilia Ngomwani, yaani nyumbani kwa Mtemi, na sababu ya kukimbia, wanogopa Mtemi hakuwapa ruhusa ya kutoka nje. Basi Mtemi alipoonana na mgoli mmoja, akamuuliza kusema : « wenzio wako wapi », naye akajibu : « sijui kule wamekimbilia ». Mtemi akasema : « Kumbe, mimi nikiondoka niye huenda kwa wanaume, hawala zenu. » Basi Mtemi Katuga akaudhika sana yule bibi yake, akampiga risasi na bastola kichwani. Bibi akafa, jina lake Lunenga. Basi wale wenzie wanawake waliokimbia wakaenda missioni kilimani kutoa habari ya kuwa mwenzao Lunenga ameuawa kwa kupigwa bunduki-bastola. Bwana wa missioni akawapa barua kwenda bomani Tabora. …..

P. Simeon Lourdel (1853- 1890) alifika Tanganyika mwaka 1878, akaenda Uganda mwaka 1883.
Akarudi Kipalapala pamoja na vijana, kama wakimbizi ; akaende kuona Mtemi Mirambo pamoja na P. Leonardo Blanc (1852-1886). Wakapokelewa vizuri na wakapata ruhusa kupita katika nchi yake bila kulipa hongo (tarehe 5.11.83)

P.Augustino Levesque (1849- 1912) na P.Ludovico Girault (1853- 1941) wakaanza safari kuenda kutafuta mahali pa kujenga stationi katika nchi ya Ukune. Tarehe 13.11.83, wakaenda kwa Mtemi Mirambo ; wakamkuta pamoja na Mwingeleza Bwana Shaw. Mtemi Mirambo akasema : « Wafaransa na Waingeleza ni marafiki na kaka zangu. ». Tarehe 18.11.83 mapadre wakafika Iwe Lya Shinga. Mtemi Mirambo akatuma habari kusema kwamba atawatuma watoto wake kusoma. Tarehe 05.12.83 P. Levesque akaandika barua kutoka kijiji cha Seru (karibu na mlima Mkungulu) kusema kwamba anapenda kukaa huko na ni mahali pazuri, lakini baada siku chache akapata habari kurudi Bukumbi.

Tarehe 03.01.1884, P. Levesque na Livinhac wakaenda kuomba tena kwa Mtemi Mirambo wapate ruhusa kujenga stationi. Mtemi Mirambo akakubali tena, na P. Lourdel akafika kwenye ikulu ya Mtemi Mirambo, tarehe 03.04, pamoja na vijana sita wa Uganda. Akamkuta Mtemi mgonjwa lakini aliwapokea na akawaambia waende Iwe Lya Shinga, siyo Seru, kwa sababu ni usalama zaidi.

P. Lourdel akafika Iwe Lya Shinga, tarehe 15.04.84 ; mara moja wakapata ploti na wakaanza kujenga tembe ya meta 15 ya urefu. P. Petro Giraud (1855- 1887) akafika tarehe 25.05. Mwezi wa saba, stationi ikaitwa « Maria Mtakatifu wa Ukune ». Vijana wakajenga tembe yao na wakaizungusha yote na ua kujilinda na Wangoni waliokuwa wengi wakiua na kuiba mali ya watu. Tarehe 11.09, Mtemi Mirambo akapita na jeshi lake kuenda Iboja kupigana na mjomba wake, Mtemi Kapela.
Tunaweza kusoma maisha ya Mtemi Mirambo katika kitabu cha P. Roger Fouquer :
MIRAMBO (nouvelles éditions latines, Paris, 1966)

Sasa tufuate maandishi ya P. Simeon Lourdel : Iwe Lya Shinga.

1884 :
Tarehe 31 octoba :Mirambo alitutumia mbuzi kwa ajili yaMarengo. Alikuwa anaumwa mafua akaomba atibiwe.

Tarehe 1 novemba :Marengo aliondoka na matabibu.Nilimuomba Mirambo samahani kwa kutoweza kwenda mwenyewe kumpatia kitubio ya kwanza ; ninaogopa kufikiriwa kuwa napigana vita hapa unyanyembe na kwingineko.Jioni nilitembea na watoto pembezoni mwa kijiji cha Henza.

Tarehe 10 novemba : Mirambo anatutumia salamu ; amepata nafuu na anakubaliana na sisi kwa kutokwenda kumtibu wenyewe. Siku hizi, kuna mapigano kwa Kapera. Kwa kuwa Kapera hakujua ni jinsi gani anaweza ondokana na Mirambo, anaamua kuwa mdanganyifu. Alijifanya anataka amani na akaomba urafiki na Mirambo, huku akisema kupambana na Watuta. Hivyo watu wake wakaanza kuimba « ndugu, ndugu » kwa watu wa Mirambo. Wito huu ulikaribishwa kwa furaha ; baadhi ya maaskari wa pande mbili walikaribiana na kuvuta tumbaku kwa pamoja.Tumbaku ilikuwa kwenye bakuli, na hii ni ishara ya amani. Wananchi walianza kusema : « mleteni Mirambo, ili aje mwenyewe kuweka masharti ya amani. » ; wanaondoka kwenda kumuita Mirambo.Mirambo bila kuwa na wasiwasi wowote kuhusu mapendekezo ya adui yake alianza safari ya kuja kwenye kundi la kwanza la maaskari.

Alikuwa amefuatwa na baadhi ya maaskari na baadhi ya Baumpa. Sehemu nyingine ya Baumpa na ya mtemi wa Ushirombo walitaka kubaki kwenye kundi la kwanza la ulinzi. Kwa bahati nzuri, hii ilimsaidia Mirambo, kwani vinginevyo yeye mwenyewe alikuwa ameisha potea.Kwani baada ya hatua chache kutoka kwenye kambi, mapambano makali yalianza nyuma yake. Vile vile mbele yake kulikuwa kundi la maaskari wamejificha, ambao walikuwa wanadai kutaka amani. Walianza kuwatumia mishale Wabompa ambao baadhi yao walikuwa wamekuja bila silaha zozote, kitu ambacho kinaonekana hakina busara.Watu watano walichomwa vibaya na kuanguka. Baada ya kuona kuwa amebanwa katikati ya makundi mawili, Mirambo alikimbilia kwenye jeshi lake. Ingawa Watuta kwa kusaidia na Kanga-kanga na Kapera walipoona Mirambo ameondoka kwenye kambi yake akiwa na karibu jeshi lake lote, walidhani watapata ushindi rahisi. Ila walishutukizwa sana na Wabaumpa waliokuwa wamebaki kwenye kambi pamoja na mtemi wa Ushirombo ; baadaye iliwabidhi kukimbia vita huku wakiacha baadhi wenzao wamekufa katika uwanja wa wita. Mtemi wa

Bukamba, akishirikina na Kapera, alipata risasi kwenye mkono ; muanangwa mmoja, ambaye ni jirani yake, amekuwa amewawa pale pale ; kati ya marugaruga yao, kumi na saba walisambaza miili ya maasakri sehemu hiyo ; Wabaumpa waipata zaidi ya bunduki ishirini na saba. Ushindi ulipatikana siku hiyo na kwa bahati nzuri ujanja wa Kapera ulikomeshwa.

Tarehe 24 novemba : Siku hizi, Mirambo aliwakataza watu kulima mwaka huu. Kwa yule ambaye alionekana kuwa anapinga maamuzi alikuwa anaadhibiwa vikali. Wakati wote ilikuwa vita kwa wanaume, na kilimo kwa wanawake mpaka tulipomshinda Kapera.

Tarehe 2 decemba : Bwana Shaw wa Urambo hakuja, niliondoka na bwana Stoxes kwenda kwenye kambi ya Mirambo, tukiwa na Horo ambaye ni mtemi mdogo wa hapa. Tunapita karibu na kijiji cha Ibanzu, baada ya masaa matatu tukiwa safari, tunakutana na Mtengenia, mtoto wa Mirambo ; anaonekana amechoka kweli. Anatusalimia huku kwa machozi yakimtoka. Tulipomwuliza juu ya afya ya baba yake, alitujibu kuwa leo Mungu amekuwa ni mbaya kwa sisi. Tulifikiria kuwa Mirambo ameaga dunia. Mtengenia akasema kwa kuwa nyinyi ni marafiki zetu, endeleeni mpaka kwenye kambi na mjaribu kurekebisha mambo.

Tulitaka kurudi nyuma, tukidhani kuwa Mirambo amefariki. Ili taarifa isijulikane, Itoro akaanza hadithi za uongo na tukaenda safari yetu. Saa nane mchana tukafika kwenye kambi ya warambo na washirika wao. Karibu na kambi, tulikutana na Waumpa wakati wakilinda ng'ombe wao. Tulipofika, tulipopelekwa na Kitamanua, mtemi wa Usagari. Alituambia kwa siri kuwa Mirambo ameondoka usiku huu, kwani alikuwa ameumwa sana. Alitupeleka ndani ya nyumba alikokuwa akiishi Mirambo ; kitanda kilikuwa wazi ; tulianza kuamini maneno ya Kitamanua. Wabaumpa walituzunguka huku wakicheka kama watoto, wakitaka kutuona na kutushika. Swali lao la kwanza, walitaka kujua kama sisi wazungu, tumetahiriwa kama wao. Ni vijana wazuri, wenye nyuso nzuri na kimo cha kuridhisha. Wana vitu vyote isipokuwa nguo za kuwaa ili wafiche uchi wao.Walitoa ng'ombe kwa watu wetu ili wagawane. Tupata vibanda viwili tuwe nafasi ya kulala usiku. Wavamuzi waliweza kujenga kizuizi karibu na ngome ya kijiji. Angalia jinsi waliyofanya : walipofika, walianza kujenga kizuizi pembeni mwa msitu, uliyoko kama kilometa mbili toka kijiji cha Kapera ; alafu siku zilizofuata, hasa wakati wa usiku, baadhi ya watu walikuwa wakienda kuchimba mashimo kwa umbali wa meta hamsini hivi. Pia wakatiwa alfajiri na mapema wakiweka miti ilioandaliwa jana yake ili kuwakinga wafanyakazi kutokana na risasi za maadui. Ndiyo maana baada ya miezi miwili hivi, huku wakijenga kambi zenye ngome, waliweza kufika pembeni mwa kijiji. Ila kazi hii haikuweza wazuia kutokea mlango wa nyuma. Kila mara usiku na mchana, kulikuwa na kujibishana risasi. Wakati mwingine japo ni mara chache baadhi ya watu walijeruhiwa.

Watemi mbalimbali waliyokuwa chini ya Mirambo walianza kuuunda kila mtu kambi yake. Mara chache ungeona mtu akienda mstari wa mbele kupigana. Wengine wanabaki chini ya kivuli au ndani ya nyumba zao wakionekana kama hawana na wasiwasi na vita. Tulipokuwa tukisikia mlio wa risasi, tulifikiria kuwa tuko katikati ya kambi ya pagazi ambayo inajiandaa kwa safari ya kesho.Baada ya kuzingira kijiji kizima, wavamizi waliweka nguvu zao zote kwenye sehemu ambayo kuna chanzo cha chemchemi ya maji cha kijiji. Mirambo alikuwa na mbinu ya kuchukua kijiji kwa njia ya kiu. Baada ya siku chache, wavamizi walifika kwenye chanzi cha maji, baada ya kupita ngome iliyokuwa ikizuia kwenda kwenye chanzo cha maji.

Ila kwenye ngome ya pili, walipokelewa na maji moto ambayo wanawake waliwamwangia kwa kutumia mitungi yao na kuwaunguza.Hil haikuwa mbaya sana. Kwani walinzi wajanja hawakukomea hapo ; wao waliwatupia vitu vinavyonuka vibaya….Hapa watu wa Mirambo

walisema : « Tukiachilia mbali risasi na maji moto, hivi vijidudu vipya ni funga kazi, hata ujanja wetu ni mdogo, hatukuweza kwenda mbele zaidi…. »

Kwa Kuwa Mirambo hayupo tena, kiti chake kitaachwa wazi. Kesho yake yake tulirudi nyumbani. Tukiwa njiani tulikutana na ndugu Shaw akiwa na dawa zake…..

Tarehe 11 decemba: Wavamizi waliachana na makao ya kijiji cha Kapera. Waliondoka bila kuangalia nyuma.Wabaumpa walipotambua kuwa Mirambo hayupo nao tena, walianza kutawanyika na mifugo yao. Wote walichanganyikiwa na kuanza kukimbia huku wakiacha nyuma chakula chao ambacho ni mtama.Mabomu ya gololi za chuma ya mzinga mdogo yalionekana mazito sana na mwishowe yalitupwa kwenye mashimo. Jioni Kanuka alituarifu kuwa Mirambo ameaga dunia, habari ambayo tulitunza kwa siri. Dalali zilionyesha kuwa amekufa kwa ugonjwa wa koo.

Tarehe 16 decemba: Kirunga alituma watu wake kutuaarifu kuwa haelewani na ndugu yake Kitamanua ambaye ni mtemi wa Usagari. Huyu nadhani alikuwa anataka kuwa mtemi wa Urambo. Kirunga alisambaza habari kuwa Kitamanua ndiye aliyemuua Mirambo kwa kumnyonga. Naamini kuwa hiyo ulikuwa ni uongo wa Kirungu ili kupotosha watu na pia aweze mshinda Kitamanua ambaye alikuwa mpinzani wake.
Tarehe 25 decemba: ubatizo wa Kindu Gabriel na John Baptiste (vijana wa Uganda)

1885:
Tarehe 20 januari: Kirungu alitangazwa mtemi. Kabla ya kutangazwa, alitakiwa kukaa pake yake ndani ya nyumba, haruhusiwi kutoka nje, anatakiwa alale chini. Haya mafungo ya kulazimishwa ni kwa ajili ya kujifunza jinsi ya kutawala watu ; hiyo anayekuwa mtemi mpya kabla hajaanza kazi binafsi, anatakiwa kupitia mafunzo hayo. Ni mila katika nchi ya Unyanyembe kwa mtemi mpya. Anawaza juu ya mambo ya dunia na wajibu mpya ; sijui kutokana na utamaduni kwa siku zote anatakiwa kulala chini na kukaa kimya… kwa kawaida mtemi mpya anatakiwa kutoka nje siku ambayo mwezi unaonekana kwa mara ya kwanza japo wengine huwa hawaheshimu taratibu huu. Ila tu akitoka nje, kila mtu anapiga vigelegele kwa furaha, huku vumbi kumbwa angani ikithibitisha furaha. Mtemi anapewa jina jipya na kutakiwa kila la heri katika utawala wake. Jina analopewa huwa mara nyingi linaendana na tabia ya mtemi mpya au kile kinochofikiria kuwa atakifanya. Jina la Mirambo lilimanisha « mauti », utadhani alitakiwa kuua watu wengi wakati wa utawala wake. Mtemi mpya amepewa jina la kawaida, anaitwa Mpanda Tsalo yaani mpandani wa mbegu, « mkulima ». Jina hili linaweza kuwa jina linaloleta amani na utulivu kwa wanyamwezi wote, ili amani ambayo watu wanhitaji iwasaidie wote siyo tu kwa kupanda ardhi yao yenye rotuba bali pia iweze panda mbegu mioyo ya watu hawa, ili neno la Mungu liweze enea.

« Iwe Lya Shinga, **Octobre 1884** : 31-Mirambo nous envoie une chèvre pour Maiengo. Il est malade d'un rhume négligé et demande du remède.
Novembre: 1- Marengo part avec le remède. Je m'excuse auprès de Mirambo de ne pas aller moi-même lui faire le reméde ; je crains que l'on m'accuse dans l'Unyanyembé et ailleurs de faire la guerre. Le soir promenade avec les enfants du côté d'Henza.

10 – Mirambo nous envoie saluer ; il s'est trouvé bien du remède ; il admet parfaitement la raison pour laquelle nous nous sommes dispensés d'aller le soigner nous-mêmes. Ces jours derniers, bataille chez Kapéra. Celui-ci ne sachant pas quels moyens prendre pour se débarrasser de Mirambo, a recours à la ruse. Il fait semblant de vouloir la paix et demande

l'amitié de Mirambo, disant qu'il est décidé à se débarrasser des Watutas ; ses gens donc se mettent à crier aux hommes de Mirambo : « Fraternité, fraternité. » Ces cris sont accueillis avec joie ; quelques soldats même de l'un et l'autre parti s'approchent près les uns des autres et prennent du tabac dans la même tabatière en signe d'amitié. « amenez Mirambo, disent les assiégés, qu'il vienne lui-même régler les conditions de la paix. » On part donc avertir Mirambo. Celui-ci ne se méfiant pas des propositions perfides de son ennemi, se mets en route pour venir dans le camp retranché jusqu'aux avant postes. La plupart de ses soldats l'accompagent, ainsi qu'une partie des Baumpas. L'autre partie des baumpas et le mtemi d'Ushirombo veulent rester au camp pour le garder. Heureusement de cette précaution, car sans elle Mirambo était perdu. A peine celui-ci s'était il avancé pour le commencement des pouparlers, que derrière lui, du côté du camp qu'il venait de quitter, s'engage une violente fusillade. En même temps en face de lui, les soldats ennemis cachés en embuscade près de ceux qui semblaient vouloir traiter de la paix, déchargent leurs fusils sur les baumpas, dont plusieurs avaient commis l'imprudence de venir sans armes ; cinq de ces derniers tombent bléssés mortellement. Mirambo pris entre deux feux se replie sur son camp où se trouvent ses munitions. Cependant les Watutas, aidés de Kanga-kanga, le mtémi du bukuné de Kapéra qui, en voyant Mirambo parti de son camp avec presque toute son armée, espérait trouver une victoire facile, sont reçus vigoureusement par les baumpas réstés à la garde du camp avec le mtémi d'Ushirombo ; bientôt même ils sont mis en fuite laisant plusieurs morts sur le champ de bataille. Le mtémi de Bukamba, allié de Kapéra, recevait une balle au bras, un muanangua, son voisin, était tué sur place, dix sept de leurs rougas-rougas jonchaient la place de leurs cadavres et vingt fusils tombaient au pouvoir des baumpas : la journée appartenait à ces derniers, et grace surtout à eux, la ruse du fourbe Kapéra était complétement manquée.

24 – Ces jours derniers Mirambo a défendu aux hommes de cultiver cette année. Celui qui est pris en contravention est soumis à une forte amende. La guerre pour les hommes, la culture aux femmes, jusqu'à ce que nous soyons vainqueur de Kapéra.

Décembre : 2 – Mr Shaw n'arrivant pas, nous partons Mr Stoxes et moi, pour le camp de Mirambo avec Itoro, le petit chef d'ici. En passant près d'Ibanzu, à 3 heurs d'ici, nous rencontrons Mtengegnia fils cadet de Mirambo ; Il a l'air tout abattu. Il nous dit bonjour les larmes aux yeux et sur notre demande des nouvelles de la santé de son père, il nous répond (mungu ietu mbaia) Dieu est mauvais pour nous aujourd'hui. Nous soupçonnons que Mirambo est mort. Cependant, ajoute Mtengegnia, vous vous êtes nos amis, allez, continuez votre route jusqu'au camp et tachez d'arranger les affaires. Nous voulions revenir en arrière, persuadés que Mirambo avait cessé de vivre, mais que, pour éviter que le bruit de la nouvelle ne fût connue, Itoro nous conta un mensonge et nous continuames notre route. A deux heures de l'après midi nous arrivons au camp des Warambos et de leurs alliés. Aux apporches du camp nous rencontrons les féroces Waumpas occupés à garder, leurs troupeaux de vaches. En arrivant nous sommes reçus par Kitamanua, mtemi d'Usagari. Il nous dit en secret que Mirambo est parti cette nuit même par ce que sa maladie était devenue très grave. Il nous introduit dans la maison même habitée par Mirambo, le lit était vide. Nous semblons croire aux paroles de Kitamanua – les baumpas nous entourent en riant comme des enfants voulant nous voir et nous toucher. Une de leurs premières questions est de nous demander si nous autres, blancs, nous sommes circoncis comme eux. Ce sont de beaux hommes, bien fait, aux traits réguliers et d'une taille très avantageuse. Il ne leur manque que l'habit pour se protèger avantageusement. On donne un bœuf à nos gens qui se le partagent. Deux petites huttes sont mises à notre disposition pour passer la nuit. Les assiégeants sont parvenus à se batir un retranchement tout près de la barricade du village.Voici comment ils s'y sont pris. En arrivant ils se mirent à faire une pallissade sur les bords de la forêt à deux km environ du village de

Kapéra ; puis les jours suivants, pendant la nuit, une partie du monde allait faire des trous à une cinquantaine de mètres en avant et de bon matin les bois, préparés de la veille, étaient immédiatement placés et protégeaient les travailleurs contre les balles des ennemis ; c'est ainsi qu'au bout de deux mois, en établissant successivement de petits camps fortifiés, ils sont parvenus jusqu'à la porte du village. Mais ce travail n'empêche pas les assiégés de sortir par la porte de derriére. A chaque instant le jour et la nuit il se fait des échanges de coups de fusil.Il arrive de temps en temps, mais rarement, qu'un homme est blessé. Les différents chefs soumis à Mirambo forment chacun leur camp retranché. Il n'y a guère que celui qui est allé en avant qui combat. Les autres assis à l'ombre d'un arbre ou dans leurs huttes ne semblent guère s'inquiéter de la guerre. Si on n'entendait de temps en temps des coups de fusil, on se croierait au milieu d'un camp de pagazis qui se préparent pour la route du lendemain. Au lieu d'entourer complétement le village les assiégeants ont porté tous leurs efforts sur un seul point du côté où se trouve la source qui fournit l'eau au village. Le plan de Mirambo était de prendre le village par la soif. Il y a quelques jours, les assaillants étaient parvenus jusqu'à la source, après avoir forcé la premiére barricade, qui en défendait l'accès. Mais à la seconde barricade ils furent reçus avec de l'eau chaude que les femmes leur jetaient dans de grandes callebasses qui se brisaient tombant sur eux. Cela n'était pas encore un très grand mal. Mais les braves assiégés ne s'en tinrent pas là, moins modérés que Cambronne qui, à la sommation de se rendre n'avait lancé qu'un mot malsonnant, ils en vinrent à lancer des faits mal odorants. Sans cela, disent les intrépides assaillants, nous étions maîtres de la place. Passe encore, ajoutaient- ils, de recevoir des balles et de l'eau chaude, mais contre des projectiles de ce nouveau genre, notre bravoure est impuissante. Nous n'allons pas tout à fait jusqu'aux avant- postes afin de n'être pas reconnus, car les gens de Kapéra supposeraient tout naturellement que nous sommes venus aussi leur faire la guerre. Maintenant que Mirambo n'est plus là, le siège va probablement être abandonné. Le lendemain matin retour à la maison. En route nous rencontrons Mr Shaw qui vient avec ses remèdes…

11 – L'armée des assiégeants a abandonné le siège du village de Kapéra. Ele s'est sauvée en déroute. Les baumpas s'appercevant que Mirambo n'était plus là, ont commencé à dégerpir avec leurs troupeaux. Aussitôt panique générale et chacun de se sauver au plus vite abandonnant leurs provisions de mtama. Les boulets d'un petit canon apporté pour renverser les barricades, sont trouvés trop lourds : on les rejetent dans des trous. Le soir Kanuka m'apprend la mort de Mirambo que l'on tient encore secrète. Il est mort d'une laryngite ulcèreuse dont sa maladie avait tous les symptômes.

16 – Kirounga envoie ses gens nous prévenir qu'il se trouve en mauvais rapports avec Kitamanua, son parent mtemi d'Usagari. Celui-çi a, je crois, des prétentions sur le butémi d'Urambo. Kirounga fait courir le bruit que Kitamanua est l'auteur de la mort de Mirambo, qu'il l'a étranglé lui-même. Je crois que ce n'était là qu'une fausse accusation que Kirounga invente pour rallier l'opinion de son côté et de la détourner de son compétiteur.

25 – Noël. Baptême de Kindu Gabriel et de Jean-Baptiste .

Janvier 1885 : 20 – Kirounga a été proclamé mtémi. Avant d'être proclamé, il a du passer quelques jours seul dans une maison couchant par terre et n'ayant pas le droit de sortir de la maison. Cette retraite forcée est de règle dans l'Unyamwezi pour les nouveaux mtémis, avant qu'ils n'entrent définitivement en fonction. Méditent-ils sur la vanité des choses humaines et les devoirs de la nouvelle charge, je l'ignore. Toujours est il que, d'après les traditions, qu'ils doivent coucher par terre et garder un absolu silence…Habituellement le nouveau mtémi ne devrait sortir que le premier jour de la lune, mais quelques-uns passent sur cette derniére

formalité. Aussitôt qu'il est sorti de la maison, tout le monde pousse des cris de réjouissance, la poudre parle, on impose au mtémi un nouveau nom et on lui souhaite toute sorte de prospérité ; le nom a souvent beaucoup de rapport avec le caractère et les aptitudes du nouveau mtémi, ou ce que l'on pense qu'il fera. Ainsi Mirambo portait bien son nom, car les nombreux cadavres dont il a couvert la terre par ses guerres incessantes, en prouvent la justesse (Mirambo veut dire cadavres), comme si son affaire à lui pendant son règne était de faire de nombreux cadavres. Notre nouveau mtémi a pris un nom plus passifique. Ils'appelle Mpanda Tshalo (cultivateur des campagnes). Puisse ce nom de bonne augure devenir le mot d'ordre de nos pauvres Wanyamwezi et que la paix que tous désirent ardemment permette non seulement de semer leurs riches campagnes des grains de la terre, mais aussi fasse germer dans leur cœur fécondé de la grace d'en haut la céleste graine de la parole de Dieu…

(+ Petit écho, 1990/9 N. 814, p.455…..)

HISTORIA YA MTEMI KAPELA WA UKUNE.

Mtemi Kapela alikuwa mtawala wa jadi katika nchi ya Ukune, ambapo kwa sasa ni Kata ya Ukune, lakini mipaka haijumulishi maneno yote ya himaya ya Kapela - mengine yako nje ya Kata ya Ukune.

UKOO WA KAPELA.

Mtemi Kapela alikuwa wa kabila la Kinyamwezi, baba yake aliitwa Kasiga ambaye alimwoa binti mmoja katika Ikulu ya Usanda kwa Mtemi Ndugulile aitwaye Masele. Lakini haifahamiki wazi kuwa alikuwa ni mtoto wa Ndugulile. Huyo Masele alikuwa mama yake Kapela. Kawaida ya watemi ilikuwa kuoa wake wengi, na watoto waliozaliwa majina yao yalifanana kwa kuwa kila alizaa na kumwita mtoto wa kiume kwa jina la babu yake. Ukoo wa Kapela ni kama ifuatavyo:

Baba yake aliitwa Kasiga, mama yake aliitwa Masele

Kapela alizaa watotot tisa : Kalonga, Kasiga II, Mwizalubi, Kasiga III wa mke wa pili, Kufumigulu, Ndwikwa I, Ndili, Nyamizi, Bugumba.

WATEMI WA UKUNE.

Utemi wa Ukune umetoka Ukimbu, walikuja watu wawili kutoka huko kutawala Ukune, nao ni :

1. Magokola aliyetawala Manungu ambayo kwa sasa inaitwa Uyogo.
2. Kifumigulu I , aliyetawala Luguma na baadaye akawa Mtemi wa Ukune wa kwanza katika himaye hii waliofuata ni :

Nkinga Kifumigulu II, Kasiga I, Nkinga, Kapela I Kasiga, Kifumigulu II, Kapela,Ndwikwa II Kapela, Kapela II Kifumigulu – na wa mwisho Ndwikwa II Kapela.




Kaburi ya mtemi Kapela na wengine

MAISHA YA MTEMI KAPELA KASIGA.

Haifahamiki wazi ni lini Kapela alizaliwa, lakini inakadiriwa kuwa alifariki akiwa na umri wa miaka 65, hivi hapo mwaka 1891, hivyo basi huenda alizaliwa kabla au baada ya mwaka 1826. Mtemi Kapela alikuwa mrefu, mweusi tii, mwili wake ulikuwa na nywele (manyoya) nyingi na alitisha sana na kuogopwa.Alikirithi kiti cha utemi kutoka kwa baba yake Kasiga aliyekuwa na ikulu nne, ikulu kuu ilikuwa Luguma , ikulu nyingine zilikuwa Iboja, Igalula, na Chona.Kapela alizaliwa katika ikulu ya Igalula.Alipotawala ikulu yake ikawa Iboja. Mtemi Kapela alikuwa mwenye tamaa ya kuwa tajiri, na utajiri wake aliupata kutokana na ushindi alioupata katika vita na kuteka nyara mali nyingi na watu pia. Silaha zake zilikuwa bunduki aina ya gobole, mikuki, mishale na pinde pamoja na madawa ya kienyeji. Dawa hizi za kienyeji zilimpatia umaarufu sana katika vita hivi, kwa mfano alikuwa na mkuki wa shaba ambao aliufungia hirizi, aliutumia wakati ule tu alipoona karibu kushindwa au kuzidiwa nguvu, aliweka bunduki chini ya mabega na kuushika mkuki wake akiyaelekeza makali yake kwa adui na adui walianguka pale pale na kufa . Jeshi la Kapela lilikuwa kubwa lililounganisha makabila mengi madogo madogo ya mkoa wa Tabora na sehemu za Kahama. Kapela aliungana na Mtemi Mirambo wa Ulyan ikulu (Ulyankulu) ambaye alikuwa ni mtoto wa dada yake –kiukoo. Mtemi Mirambo alikuwa kama mkuu wa majeshi ya Kapela. Baadaye Mirambo naye aliunda jeshi lake binafsi na hatimaye akapigana na mjomba wake.

USHIRIKIANO WA MIRAMBO NA KAPELA KIVITA.

Mtemi Mirambo alikuwa mtawala katika nchi ya Unyanyembe. Kabla ya kuwa Mtemi, hapo mwanzo alikuwa ni mpiganaji na jemadari wa Mtemi Ntinginya wa Usongo. Alipoona amekuwa na uwezo wa kutosha wa kivita aliamua kuunda jeshi lake ambalo ni la Tabora.

Baadaye aliposikia mjomba wake analo jeshi lenye nguvu kubwa, aliamua kuja Ukune kuungana na mjomba wake. Kwa kuwa Mirambo alikuwa mpwa wa Kapela, ilibidi awe chini yake, akapewa cheo cha kuyaongoza majeshi yote. Baada ya kushirikiana na Mirambo, Kapela alikuwa shujaa sana, lakini mpwae Mirambo, hakupendezwa na muungano huu, kwani akatafuta sifa tu, hivyo aliasi na kufanya njama ya kutaka kumuua mjombe wake Kapela. Katika ushirikiano wao, Mirambo na Kapela walikwenda kupigana vita Ufipa na Kigoma. Katika safari yao, Kapela na majeshi yake alipitia Kasulu, Kibondo na hatimaye Kigoma. Mirambo alipitia Mpanda. Lakini Kapela hakupigana vita kule Kigoma kwa sababu yake alikuwa ni kutoka Kigoma, hivyo basi, kwa maneno mengine ni wajomba wake. Wakati anarudi alikutana na mpwa wake Mirambo katika mto Maragarasi, kila mmoja na jeshi lake.Hapa tena kulitokea mabishano nani atangulie kuvuka. Baadaye waliamua wote wawili wapande mtumbwi na ndipo wakavuka. Na hapa Mirambo alitaka kumuua Kapela naye aligundua njama hiyo .Walipovuka majeshi yote yalielekea ikulu kwa Mirambo kunakoitwa Ikonongo.Kapela alipiga kambi yake mbali kidogo nje ya ikulu ya Mirambo. Mirambo aliwaarifu wake zake ambao walikuwa zaidi ya mia mbili kuwa amekuja na mjomba wake Mtemi Kapela, hivyo walienda kumsalimia wote kwa pamoja wakawa wamepanga mstari.

Wake wawili wa kwanza walitangulia, mke wa kwanza (Wipunga) ambaye huvaa « shilungu » shingoni na mke wa pili huvaa shilungu cha shaba aitwaye Mihopa, wote walichukua nyundo moja moja. Mke wa kwanza huku alichukua meno mawili ya tembo na yule wa plil jino la tembo kama zawadi kwa mkwe wao. Siku iliofuata Kapela aliamua kurudi nyumbani kwake Ukune baaba ya kuagana na Mtemi Mirambo.

VITA VYA USUKUMANI.

Baada ya siku chache Kapela aliporudi nyumbani kwake, kutoka Ikonongo, Mirambo alituma habari kwa mjomba wake Kapela kuwa ajiandae maana anakuja kumsaidia kuwpigana na maadui wake.Kapela alikubali kupewa msaada huo. Mirambo alikuja na jeshi lake hadi Ukune katika Ikulu. Akapiga kambi yake katika mlima wa Mangua. Kapela akamwambia Mirambo kuwa safari yao ni kuelekea Usukumani kupita Ukamba, Luhombo na Tinde.

Walipofika katika mpaka wa Tinde na Usanda, Mirambo alisema kuwa yeye atapitia njia ya Shinyanga na Kapela apitie Nindo na kukutania Usumau. Mirambo alikuwa na fununu kuwa sehemu za Usia kuna ngombe wengi wa Wasukuma.Hivyo alikusudia kuteka nyara ng'ombe hao. Kapela alimwambia Mirambo kuwa ukifika Usanda asipige eneo hilo kwa kuwa huko kuna wajomba zake .Safari ya Mirambo haikuwa na mafanikio yoyote kwa kuwa Wasukuma walikuwa wamepata habari kuwa Mirambo atapita kuchukua ngombe wao. Wasukuma waliwaficha ng'ombe wao porini, Mirambo akaambulia wanawake tu. Akaendelea mpaka Seka huko alikuta kundi kubwa la ngombe ambao walikuwa ni wa Mwanamalundi, mtu maarufu sana kwa uchawi. Mirambo akashindwa kuwachukua na askari wake wengi wakafa kwa madawa ya mchawi huyo na kwa sababu ya njaa. Mirambo alienda moja kwa moja mpaka Usumau ambako waliahidiana kukutana na Kapela sehemu iitwayo Bungulwa . Kapela alifanikiwa kuteka ngombe wengi akiwemo ngombe dume wa mizimu wa Msukuma wa Nela .Ngombe huyo alikuwa anaitwa Ilindilo, yaani ngombe wa kulinda nchi. Mirambo akamwambia Kapela kuwa nimemkuta Msukuma moja huko ni mchawi kamaliza askari wangu Akamsimulia habari zote za Mwanamalundi. Mirambo aliona wivu kuwa yule ngombe dume na kuapa kuwa lazima amchukue. Kapela na Mirambo walikaa muda mrefu Usukumani Nela, Usumau na Uhungukila. Na walifaulu kuteka mali nyingi ng'ombe wengi pamoja na watu pia.

KAPELA NA MIRAMBO WANARUDI NYUMBANI.

Vita vya Usukumani vilipomalizika walirudi kupitia Ngaya, Kahama na kufika Ukune. Mirambo akafika kwenye kambi yake ya Mangiwa. Baadaye akamtuma tarishi wake aende kwa Kapela kuchukua ng'ombe wa kitoweo – akapewa ng'ombe 45. Mirambo akamtuma tena tarishi kuendea ngombe na akapewa ng'ombe 25. Akamtuma tena safari ya tatu, Kapela alikaa kimya hakumjibu kitu.Tarishi akarudi kumweleza Mirambo. Mirambo akamwambia kuwa labda hakusikia, arudi tena. Tarishi akarudi mara nyingine vivyo hivyo hakupewa jibu. Mirambo akamtuma tarishi kuwa akamwambie Kapeka kuwa wakutane kesho yake .Mtemi Kapela alikubali kukutana na Mirambo. Kesho yake wote wawili walikutana wakiwa na majeshi yao. Mirambo alidai apewe ng'ombe zaidi na Kapela akamjibu kuwa nimekwisha kukupa ng'ombe wengi, wote hao, huna shukrani tu. Nia ya Mirambo ilikuwa kumpata yule ng'ombe (Ilindilo) kwa hiyo ng'ombe aliokuwa akiwapata hakuwemo Ilindilo.

Alipoona hampati alizidi kudai ili atimize azima yake ya kumpata Ilindilo Baada ya mabishano makali, Mirambo akamwambia Kapela kuwa anakwenda kujenga Isela Magazi lya Wapela (yaani mtiririko wa damu ya wafuasi wa Kapela) na akimshinda, Kapela atachukuwa wake wa Mirambo na mali yake yote. Kapela naye akawambia Mirambo kuwa atajenga Iboja Mishinzi ya Balambo, naye akimshinda atachukua wake wote pamoja na mali yake. Msemo huu wa Mirambo wa kujenga Isela Magazi lya Wapela na ule wa Kapela wa kujenga ngome ya Iboja Mishinzi (yaani ng'ome ya kuozesha nywele za wafuasi wa Mirambo) maana askari wa Mirambo walikuwa hawanyoi nywele, tunapata majina ya Iboja - ikulu ya Kapela ambalo ni jina linatumika mpaka hivi leo, na lilo la Isela Magazi linatumika hadi leo. Katika ujenzi wa ngome ya Mirambo aliyoiita Isela Magazi, alizungushia handaki, shimo refu na pana, kati kati na pembeni. Kapela alijenga ngome ya Iboja, akazungushia kuta

sita za miti iliyochongwa juu na kuwa na makali. Kuta hizi sita hazikuwa zimeungana. Na pembeni mwa kuta hizo zilijengwa nyumba za maaskari. Kuta hizi za miti zenye ncha kali lengo lake lilikuwa kwamba mateka na maiti wa askari wa Mirambo walikatwa vichwa vyao na kutundikwa juu ya ncha kali za miti hiyo, na hivyo hakukamilisha lengo na maana ya Iboja mishinzi.

MIRAMBO AANZA VITA NA KAPELA KATIKA NCHI YA UKUNE.

Baada ya watemi hawa wawili kukamilisha ngome zao za vita, Mtemi Mirambo akatuma habari kwa mwanangwa (mjumbe) aitwae Malungi kumshawishi wamgomee Kapela, Malungi alikuwa anakaa Ilumbu, naye kishafariki. Ujumbe mwingine ukapelekwa katika kijiji cha Nhulu kwa mwanangwa Mpenuki naye akakubali, hali kadhalika mwanangwa wa kijiji cha Bunanzaba, Nhanga akakubali kumgomea Mtemi wao Kapela. Kadiri ya maelezo ya Mtemi wa mwisho (aliyepo sasa) Ndwikwa Kapela II ni kwamba, wakati ujumbe wa kutoka kwa Mtemi Mirambo unajadiliwa kuhusu swala la kugomea Mtemi Kapela, mikutano hiyo ilifanywa hadharani wakiwemo na raia (wazengi). Na ilidhihirika kwamba raia hao walikubali kwa shingo upande tu maamuzi ya wanangwa wao. Baada ya wanavijiji wa Nhimbo na Nhulu walichukua mavi ya ng'ombe aliyechinjwa na kuyapeleka kwa Mtemi Kapela kama ushahidi ya kuwa Mtemi Mirambo kafika kijijini kwao na akachinjiwa ng'ombe kwa ajili ya kitoweo.

Na katika kijiji cha Kilimbu kadhalika walisema hivyo, pamoja na hayo Mtemi Kapela akawaabia kuwa kafika katika vijiji vyao, na kufanya mikutano na raia wote .Watu walialikwa na kufika mkutanoni, Wanangwa hawakufika, walijificha ndani, hivyo mtemi aliamrisha askari wakamatwe na kuletwa mkutanoni na baadaye walinyongwa hadharani isipokuwa mwanagwa wa Bunzamba hakuwa na matatizo. Mtemi Mirambo alipoondoka Ulyankulu na kuja Ukune na akapiga kambi katika kijiji cha Sole. Hapo ndipo akatuma ujumbe kwa vijiji alivyoshauriana navyo. Wajumbe walipofika katika vijiji vya Nhulu na Kilimbu wakakuta watu walishahamishwa kijiji cha Igalula. Wakaenda katika kijiji cha Bunzaba kwa Mwanangwa Nhanga, na kuleta ujumbe wa kutoka kwa Mirambo, lakini akajibu kuwa yeye siye Nhanga balini Ndasa ya tembo ya kulala na Mirambo yaani ni tembo tasa wa kulala na Mirambo ndipo wajumbe wakamuliza kuwa, je yuko tayari kupigana na Mirambo ? ajibu na kusema yuko tayari.

MIRAMBO ANAOMBA MISAADA KWA WATEMI WA UKAMBA NA WENGINE.

Wajumbe wa Mirambo walirudi na mambo yote waliyoyaona na kuyasikia na kwamba Nhanga yuko tayari kupigana na Mirambo. Mirambo alipopata taarifa hiyo alichukia sana. Ndipo Mirambo akaenda kwa Mtemi Magope wa Ushetu, ikulu la Itulamashiki. Mtemi Magope alikataa kwa kuwa alikuwa kamuoa dada wa Kapela, aitwae Mboboto. Na inasimuliwa kuwa huyo Mboboto alikuwa ni dada yake Nyakazi mama wa Mtemi Mirambo, baba mmoja na mama mmoja. Mtemi Mirambo baada ya kukataliwa akaenda kwa Mtemi Lembeli wa Bulungwa, akiomba ushirikianao wa kivita dhidi ya Kapela, Lembeli akakubali kwa shingo upande. Usiku wa manane alienda kwa siri kwa Mtemi Kapela, alikimbia kutoka Bulungwa. Kapela alimpokea na kumpeleka Igalula. Mtemi Mirambo hakuishia hapo, bali alikwenda kwa Mtemi Ntinginya kule Ubagwe. Ntinginya alikataa kwa sababu Kapela alioa binti yake aitwaye " Nulishe Ntinginya" ; Ntinginya kuona hivyo akaamua kukimbia ili asishuhudie ugomvi huo na mkwilima wake. Akakimbilia kijiji cha Isevya huko Tabora. Mtemi Mirambo kuona hivyo kwa kukosa msaada akarudi na kupitia kwa adui yake Ndasa na kumwambia kuwa kesho tutaanza mapambano. Ndasa alikesha akiwachanja dawa za kinga askari wake. Dawa hiyo inasimuliwa kuwa ilikuwa na kinga ya risasi kutopenya mwilini.

Kulipopambazuka tu majeshi ya Mirambo yakaanza mashambulizi. Vita hivyo vilianza wakati wa majira wa mwanzo wa kiangazi, mwezi wa nne au wa tano. Ulipofika mwezi wa nanne, Kapela akatuma mjumbe kwa Ndasa kuwa ampishe Mirambo ili aende kwa Mtemi Kapela. Ndasa alipokea ujumbe huo na mara moja akaondoka hadi kwa Kapela na majeshi yake. Ndani ya ngome yake akamwacha mtu moja kipofu. Mtemi Mirambo alipofika hakukuta watu katika ng'ome ile isipokuwa yule kipofu na kumuuliza, je "wamekwenda wapi watu wote " akasema kuwa wamekimbilia kwa Mtemi Kapela, Iboja. Mtemi Mirambo kuona hivyo alirudi Sole katika ngome yake. Huo ndiyo ukawa mwisho wa vita kati yake na Ndasa. Mtemi Mirambo alikuwa na ngome nyingine huko Ukune katika kijiji cha Iwe lya Shinga, ndiko alipompelekea mama yake baada ya baba yake kufariki, akiitwa Mtemi Kasanda. Lakini wakati huo vita kati yake na Ndasa, mama yake alikuwa tayari kisha fariki na kuzikwa pale pale Iwe lya Shinga. Huko alibaki mama yake mdogo aitwae Masele. Na huko Mirambo alijiandaa kwa vita kati yake na Mtemi Kapela mjomba wake.

MTEMI MIRAMBO AFANYA MATAMBIKO KABLA VITA.

Padre Simeon Lourdel wa Shirika la Mapadre Weupe (White Fathers) ambae wakati huo alikuwa rafiki yake Mirambo, katika kitabu chake kinachosimulia kuwa « askari wa Mirambo wakati wanacheza ngoma ya ibada ya matambiko walikuwa wamevaa manyoya ya mbuzi mabegani, walikuwa wakiimba « Kapela ufililie mbali, Kapela ufifilie mbali… » Walirudia rudia maneno hayo. Mirambo alipomuaga mama yake mdogo Masele kwamba anajiandaa kwenda kupigana na Kapela. Mama yake akamshauri kwamba « mwanangu usiende kupigana na Kapela kwa kuwa ni mjomba wako na huko ndiko nyumbani kwetu »..

Mirambo akamjibu « mama acha, kama unamtetea nenda kujiunga na wachawi wenzako akina Subi » (Subi alikuwa ni dada yake na Kapela pamoja na mama yake Mirambo – Nyakasi, na Masele mdogo wao) Baada ya matambiko, Mtemi Mirambo na askari wake waliondoka kwenda vitani, wakafika katika kambi yao ya huko Manguwa. Kabla hajaanza vita Mirambo alikwenda kuomba msaada kwa Watemi wa Kahama, akianzia Ushirombo kwa Mtemi Makaka, naye akakubali. Kisha akaenda kwa Mtemi Mugunga wa Mbogwe. Lakini yeye alikataa kwa kuwa mtoto wa Kapela alikuwa ameoa mtoto wake. Inasemekana kuwa wakati Mtemi Mugunga alipokea ujumbe kutoka kwa Mirambo alikuwa kainamisha kichwa kwa Mirambo. Mirambo alipandwa na hasira, akachomoa kisu na kumkata kichwa na kufa papo hapo. Mirambo akatawaza mtoto wake na Mugunga wa miaka saba, kisha akaondoka kwa Mtemi Sundi wa Nsalala – Ngogwa. Sundi alikubali kumsaidia. Mirambo akaenda Isaka kwa Mtemi Maweda. Maweda alikataa. Mirambo alipokataliwa alianza kupigana hapo hapo na Mtemi Maweda.

MTEMI KAPELA AKAPIGANA NA MTEMI SUNDI.

Kapela alipoona kuwa adui yake anazugumza zugumza kutafuta misaada naye akaondoka kwende kuomba msaada kwa Mtemi Sundi wa Ngogwa. Alipofika kwa Sundi akaelezwa habari za Mirambo, hivyo Kapela akamua kuanza kupigana vita. Mirambo aliposikia kuwa Kapela anapigana na rafika yake, akaacha kupigana na Mtemi Maweda, akaenda kwa Mtemi Nkandi na kumwambia kuwa afunge njia ili Kapela asirudi kwake Ukune. Mirambo akaanza kukishambulia kijiji cha Kigwa kwa Mwanangwa Nkunda na kukichoma moto. Wakati huo Mtemi Kapela akiendelea na vita vyake. Mirambo akakishambulia kijiji kingine cha Luguma kwa Mwanangwa Hanga na kukichoma moto. Kapela aliposikia kuwa nchi yake kinashambuliwa akaamua kurudi ili kutetea nchi yake. Alipokuwa akirudi alikuta njia imefungiwa na Mtemi Nkandi wa Zomgomela, njia ipitayo katikati ya milima miwili, majeshi ya Nkandi yalikuwa katika eneo hilo. Kapela alipoomba njia, aliambiwa aache ya jana na afuate ya leo. Kapela akamuuliza Nkandi « je unataka tupigane vita ? » Nkandi akasema

yuko tayari. Mirambo akamwambia kuwa jambo hili limetoka mbali litaharibu uhusiano wetu bure Nkandi akamwambia kuwa « nimekuambia acha ya jana na tufuate ya leo ».

VITA KATI YA KAPELA NA NKANDI.

Baada ya mabishano ya muda mrefu, mapambano yalianza majira ya saa saba mchana. Ilipofika saa mbili hivi usiku, giza lilikuwa limeingia. Hapo Kapela akapenya akakimbilia mlimani, mlima wa Mikome, na akaona shimo (pango) lililochimbwa na wanyama na kujificha humo. Nkandi akaamrisha jeshi yake kuzunguka mlima na kuchoma moto. Baada ya moto kuunguza mlima hadi kileleni na wao kufika mpaka huko juu ya mlima. Lakini moto haukumzuru Kapela katika lile shimo. Majsehi ya Nkandi yalipopita lile shimo, Kapela akatoka shimoni kuelekea walikotoka askari wa Nkandi. Wakati huo askari wa Kapela walikuwa wamepenya na kuenda kutoa habari Iboja kuwa Mtemi ameuawa. Lakini usemi huo ulikanushwa na dada yake Kapela, Subi. Kapela alifaulu kujinasua kutoka majeshi ya Nkandi, na alipokaribia kijiji chake alifyatua bunduki yake na mlio wake ukafika mpaka ikulu yake (Iboja), watu walikuwa wakijua mlio wa bunduki ya Kapela, walitoka kumlaki Huku wanawake wanapiga vigelegele na ngoma za utawala zilizoitwa ngoma za Mirango.

Mirambo aliposikia ngoma zikipigwa alijua kuwa Kapela amefika, akashangaa na kujiuliza, je, amefikaje wakati alimwambia Mtemi Nkandi afunge njia. Kwa hiyo aliona kuwa Nkandi amehadaa uhusiano wa Kapela na Nkandi ukawa mbaya. Wakati huo Mtemi Mirambo hakuwa na imani tena na Watemi wa Kahama. Akatuma mdogo wake aende Tabora kuwaeleza Watemi wote waliokuwa chini yake, wakusanye majeshi yao ili waje kujiunga naye.

Watemi waliofika kutoka Tabora ni hawa wafuatao:
Mtemi wa: Upimbwe, Ushisha, Ushindi, Uyowa, Ulila, Utimbwe, Itembe, Nhwande Usangi, Ukumbi, Uyogo-Tabora, Usongo-Nzega.

Watemi waliotoka Wilaya ya Kahama walikuwa hawa wafuatao:
Mtemi Makala wa Ushirombo; Mtemi Sundi wa Ngogwa; Mtemi Nkandi wa Zomgomela Mtemi Malembeka wa Ngaya hakuungana katika vita hivyo kwa kuwa alikuwa kamuoa Subi Na Mtemi Ntinginya wa Ubagwe naye hakushiriki vita hivyo kwa sababu Mtemi Kapela alikuwa kaoa kwake, mtoto wake akiitwa Hulishe Ntinginya.

Kwa kuwa Mtemi Mirambo hakuwaamini sana Watemi wa Kahama, hakuwaweka mstari wa mbele katika mapambano, bali aliwapa kazi ya kuchimba mahandaki tu.Handaki moja lilichimbwa kuanzia Manguwa kuelekea Iboja ndani. Msimamizi wa kuchimba handaki hilo akawa Mtemi wa Ushirombo –Makala. Handaki hilo linaonekana hata leo.

Watemi waliomsaidia Mtemi Kapela ni hawa wafuatao:
Mtemi Isike Kiyungi wa Unyamwezi na rafiki yake Mpangalala ambaye alikuwa Mgoni kutoka Songea.

VITA KATI KAPELA NA MIRAMBO VYAANZA.

Mtemi **Ndwikwa Kapela II,** amesimulia kuwa : Kapela alikuwa na tabia ya kutambikia kwanza kabla ya kuanza vita, wakati anajiandaa kupigana na Mirambo alifanya hivyo hivyo Aliwaalika « Waswezi », viongozi wa kuomba mizimu. Aliwaalika na wakaenda kwa Kapela na kuingia katika kijumba cha matambiko (kagondo) wakakaa humo usiku kucha wakiwa pamoja na Kapela mwenyewe. Kulipopambazuka aliwapeleka kwenye mti uliopandwa juu ya kaburi la watoto wake ambao walikuwa mapacha, (Kulwa na Doto).

Waszezi wakazunguka mti huo huku wamevaa mavazi yao ya kutambikia kichawani (kishingo). Pia askari walileta silaha zao na kuzisimika chini ya mti huo. Kisha kiongozi na waswezi aliwapulizia maji yaliyochanganywa na mtama (kafupa) kuwaombea dua la ushindi. Mtemi Kapela wakati wa maandalizi yake ya vita alikwenda Kigoma na kupata pembe pamoja na mkuki alivyovitumia vikiwa na dawa. Pembe hilo alilitumia kuonyesha ishara ya hatari. Aliliweka katika mlango wa ikulu (Luzonzo), wakati wa hatari lilikuwa likivuja damu na akilikuta linatoka maji alijua kuwa hakuna hatari yoyote. Waswezi walitunga wimbo kulisifu pembe hilo wakiimba : « Nalini pembe lyane nalifunya kule ma Bhuha ulu wahaya kubuma ng'wafurani na kuloga lusalo » wimbo huo ulifahamisha sana kwa Wanyamwezi hadi leo hii. Mkuki na aliutumia alipokuwa akitembelea maeneo ya vita - ulikuwa umefungiwa hirisi katika ncha za makali yake, akikutana na adui yake ana kwa ana aliuelekea makali yake kwa adui na huyo alikufa pale pale. Mtemi Ndwikwa Kapela II (ambaye kwa sasa anaitwa George Ndwikwa Kapela II, baada ya kubatizwa katika kanisa Katoliki) husimulia kuwa vita vilianza mwezi octoba mwaka 1883, na vilidumu kwa mwaka mzima. Mtemi Mirambo alikuwa amechimba handaki lililoanzia kijiji cha Manguwa, huko Igalula ambako ndiko kulikuwa na kambi ya Mirambo. Tarehe 1/2/1883 majeshi ya Mirambo yakitokea upande wa kaskazini yalikaribia ikulu ya Kapela karibu na Posta kwa sasa. Kapela alipoona kuwa karibu Ikulu yake itatekwa, akatumia mbinu na kuwaambia askari wake kuwa wapige kelele wakisema « ndugu, tuache vita » Majeshi ya Mirambo yakaamini kweli mjomba wake anaomba waache vita kwa kujali undugu. Kulikuwepo jemadari wa Kapela, mtoto wa Subi alipoona mbinu hizi zinafanikiwa, waliwasongelea askari wa Mirambo na kuanza kuwashambulia kwa bunduki. Mtoto huyu wa Subi aitwaye Fuzigwalyuba, ndiye alyeanza kufyatua risasi, na baadaye askari wa Mirambo wakabana na kumpiga risasi na kufa. Kapela aliposikia kwamba mtoto wake amekufa, akalia na kusema « Namala bhanhu » yaani nimemaliza watu. Dada yake Subi akawaambia kuwa, « kumbe wewe bado ni mtoto, nyamaza, tutakapoipata maiti yake, tutakuwa tumeshinda ». Basi majeshi ya Kapela yakafanya juu chini yakafaulu kuipata ile maiti na kuipeleka ikulu. Palipokuwepo na wazee wanawake ambao Kapela aliwatumia kama wachawi wake wakati wa vita, nao ni :

Ngoboizizi, Wadumwa, Kabula Shingona. Wazee hawa walikuwa wanaambatana na Subi kwa kazi zao za kichawi. Subi alichukua tunda la mti uitwao mwicha – akalipakata kama mtoto na kumbembeleza na kusema « nyamaza Mirambo », wale wazee wengine wakawa wanapiga vigelegele, wakichukua pia dawa ambayo iliwafanya wasionekana mpaka kwenye shimo ambalo alikuwa akilitumia Mirambo kwa mapumziko. Wakamkuta humo ndani na kumchukua kichawi na kumpeleka kwa Kapela. Walipomfikisha kwa Kapela, akachinjwa mbwa mweusi na nyama yake ikachanganywa na sehemu kidogo ya Fuzigwalyuba na kutayarishwa kitoweo. Wakati maandalizi yanafanywa ya chakula hicho, Mirambo alikuwa kikalishwa kwenye kiti pamoja na Kapela mjomba wake akiwa hajifahamu, Chakula kilipokuwa tayari alipelekewa Mirambo ; na kuanza kula, mara akapata fahamu na kumuona Kapela ana kwa ana, ndipo Subi akamwambia Mirambo « kula tu mwanangu, hapa upo nyumbani kwa wazazi wako ». Subi akamwuliza Kapela « je una lolote la kumwuliza huyu ndiye mpwao » Kapela akamwuliza Mirambo « Mpwa wangu umeamua kweli kupigana vita na mimi mjombao ? » Mirambo hakujibu neno. Na Mirambo hakupata tena akili akawa amepotewa na fahamu. Subi akamuliza Kapela kaka yake « vipi utamfanya nini mpwao ? »

Kapela akasema « ni lazima nimuue ». Akaagiza afungwe kamba shingoni - wale wazee « wa kike » (wanawake) wakasaidiana kuvuta ile kamba na kuifunga juu katika boriti ya nyumba. Subi akachukua « ki-chungu » kidogo knaitwa « shindye » na kukinga mkojo wa Mirambo na kumpa Kapela anywe kidogo. Baadaye mwili wa Mirambo ukashushwa chini na

kichwa chake kikanyolewa nywele. hizo nywele na mkojo vipo hadi leo hii. Huo ndio ukawa mwishao wa Mirambo.
Baada ya Mirambo kufa, Subi pamoja na wale wazee wawili wakaibeba maiti bila kuonekana na kuirudisha katika handaki lake, katika sehemu inayoitwa Kundikili. Wakamlaza na kuonekana akiwa amelala. Inasemekana kwamba kifo cha Mirambo kilikuwa cha kunyongwa tarehe 2/12/1884, siku ya alhamisi. Kifo cha Mirambo katika maelezo haya kinataufautiana na maelezo yaliyomo katika kitabu kilichoandikwa na Padre John Kabeya. Maelezo yaliomo katika kitabu cha Kabeya yanamwelezea Mtemi Mirambo, lakini katika maelezo haya ni maelezo hasa ya Mtemi Kapela na maisha yake. Hivyo basi haya yote yamepatikana huenda kwa sababu ya kumsifia Mtemi Kapela na yale ya Kabeya ilikuwa kumsifia Mtemi Mirambo. Kila upande unasimulia sifa na ushujaa wa Mtemi anayehusika. Ni jambo la kutia moyo na kutoa nafasi ya uchunguzi zaidi kwa wataalamu wa fani ya mambo ya kihistoria na ya kale kutafuta maelezo sahihi ya Watemi hawa wawili. Mirambo akiwa amelazwa katika handaki lake si hai tena, majeshi yake hayakufahamu bado kama amekufa ; kesho yake asubuhi yalijiandaa kwa mashambulizi kuelekea ikulu ya Kapela. Baada ya kuona kuwa Mirambo anachelewa kutoka, hapo ndipo mdogo wake na Mirambo aitwaye Mpanda Chalo akatumwa na Ntinginya ili akamwambie Mirambo waanze mashambulizi. Mpanda Chalo alipoingia katika handaki akakuta Mirambo kisha kufa. Akapeleka habari kwa Mtemi Ntinginya kuwa Mirambo ameshakufa. Basi hapo Mtemi Ntinginya akasema kuwa sasa hakuna haja ya kuendelea na vita - Mungu kishaamua. Mpanda Chalo asema kuwa : “ kwa kuwa mimi nipo vita vitaendelea tu”. Ntinginya akasema :“ sisi tulikuwa na mkataba na Mirambo wa kumsaidia lakini sio wewe, hatukujui !”

MWISHO WA VITA VYA MIRAMBO NA KAPELA.

Mara tu baada ya kifo cha Mirambo, Watemi wote waliokuja kumsaidia Mirambo walikusanya majeshi yao yote na kuyaamuru kurudi nyumbani. Wakati huo Mapadre wa Shirika la Mapadre Weupe ambao walikuwa marafiki wa Mtemi Mirambo wakiongozwa na Padre Simeon Lourdel, walifika kumletea dawa Mirambo ya ugonjwa wa madonda ya koo. Habari za kuaminika zinasema kuwa Mirambo alikuwa na magonjwa mengi. Padre Lourdel aliunga mkono maelezo ya Mtemi Ntinginya wa Usongo ya kusisitisha mapigano.

Wakateuliwa watu wa kubeba maiti ya Mirambo na kuirudisha Ulyankulu, katika ikulu yake ya Ikononngo, kupitia Ngokolo (Iwe lya shinga), wakaongozana pamoja na Padre. Walipofika Iwe Lya Shinga, mama yake (mdogo) aliipokea maiti, kisha Padre akafanya ibada ya marehemu.Baadaye maiti ikapelekwa Ushetu katika ikulu ya Mtemi Magope, iitwayo Itulamashiki. Magope akaiosha maiti ile kuonyesha uhusiano waliokuwa nao kati yake na Mirambo. Mara baada ya tukio hilo safari iliendelea hadi Ulyankulu katika ikulu ya Mirambo, Ikononngo. Mrithi wa Mirambo alikuwa mdogo wake Mpandachalo.

KAPELA ANAYAAGA MAJESHI YAKE.

Mtemi Kapela alipothibitisha kuondoka kwa majeshi ya Mirambo na washirika wake, naye akawakusanya Watemi wote waliokuwa wakimsaidia na kuwaaga. Alitoa shukrani kwa wote waliomsaidia kijeshi na kwa kumpatia chakula hasa kutoka Mwanza na Shinyanga pamoja na Nzega. Nao ni kama wafuatao (majina ya Watemi hayakutajwa bali sehemu walizotoka tu)
Watemi kutoka: Luhombo, Tinde, Usanda, Samuye, Usia, Kizumbe, Nela, Usumau, Salawi na Nindo.
Watemi kutoka Nzega ni Watemi wa Kalitu na Mwakalunde.

KAPELA ALIPIZA KISASI KWA WALIMSAIDIA MIRAMBO.

Mtemi Mpandachalo alipochukua nafasi ya Mtemi Mirambo, Kapela akaona nafasi nzuri ya kulipiza kisasi, akaenda pamoja na rafiki yake Mgoni aitwaye Mpandagalala. Wote wawili walikuwa na visasi. Kwanza Kapela mtoto wake aliyeitwa Fuzigwilyuba aliuawa na majeshi ya Mirambo. Pili, mtoto wake na Mpangalala aliyekuwa kaolewa na Mirambo – Mirambo aliamuua kwa sababu baba kake Mpangalala alimgomea kuungana naye katika vita vyake na Kapela, badala yake akamsaidia Kapela. Majeshi ya Kapela na Mpangalala yakashambulia ikulu ya Ikonongo na kumkamata Mpandachalo na kumuua. Kawaida ya vita hivyo vya kienyeji ni kwamba kiongozi au Mtemi akiuawa, maana yake vita vimekwisha.

Mara tu baada ya vita hivyo vya Urambo kumalizika, Kapela alirudi nyumbani kufanya maandalizi ya kulipa kisasi kwa Mtemi Ntinginya wa Usongo ambaye alikuwa akimsaidia Mirambo na kufaulu kuchoma ngome yake. Kapela akaenda Usongo na majeshi yake na kuizunguka ikulu ya Ntinginya - bahati nzuri alikuwepo Mzungu moja, jina lake, Stoxes, akatoa bendera ya amani na kumtaka Kapela asiishambulie ikulu ile kwa sababu alidai kuwa kulikuwa na vitu vyake vilivyoletwa kutoka Ulaya, vikiharibiwa jina lake litakosa umaarufu huko Ulaya - Kapela akaamua kuacha kuishambulia na kurudi nyumbani Ukune.

Ili kutimiza azma yake na kulipiza kisasi, hakuishia hapo, kwa kuwa bado kuliwa na adui yake mwingine ambaye alimfungia njia alipokuwa anatoka kupigana na Mtemi Sundi wa Ngogwa, kwa mashauri ya Mirambo. Huyu si mwingine bali Mtemi Nkandi wa Zomgomela – Kahama.Kapela akaenda kuishambulia ikulu yake – Nkandi kuona hivyo, akakimbilia Kahama katika mlima uliopo nyuma ya kituo cha polisi ambapo kuna tenki la maji.Wakati huo majeshi ya Kapela yalijuwa Mwime, kusini –mashariki ya maji ya Kahama.

Nkandi alipokimbia, mapambano yaliongozwa na mtoto wake, jina lake Kishimba, alitafutwa na kukamatwa na alikatwa kichwa - kichwa chake kikapelekwa Iboja.Hii ndiyo ilikuwa vita ya mwisho ya Kapela. Yule Mzungu mfanya biashara, aliposikia ya kwamba vita vimekwisha na mshindi ni Mtemi Kapela wa Ukune, akamletea zawadi zifuatazo: kwanza, bendera ya ushindi, pili kitabu cha sheria, na tatu kiti cha chuma, ambacho kipo mpaka hivi sasa. Kisha Bwana Stox akatoa ushauri kwa Watemi wote wa Tanganyika, wawe wanafanya mikutano yao huko Ukune ; ili kutumia kitabu cha sheria ya Watemi ambacho alikabidhiwa Mtemi Kapela Kasiga wa Ukune.

KIFO CHA KAPELA.

Mikutano hiyo aliyoiagiza Bwana Stoxes iliendelea kama kawaida, hatimaye Mtemi Kapela aliugua magonjwa ya kawaida tu na kufariki mwaka 1891, akiwa na umri wa miaka 65 hivi.

UTAWALA WA KIFUMIGULU II.

Kapela alipokufa alitawala mtoto wake Kifumigulu II. Wakati huo Bwana Stoxes akaja kwa Kifumigulu kuomba msaada wa ulinzi kwa safari yake ya kuelekea Kigoma. Mtemi Kifumigulu na majeshi yake waliandamana naye. Bahati mbaya, huko njiani Bwana Stoxes alipatwa na ugonjwa unaosababishwa na ndorobo, hadi kumuua. Mtemi Kifumigulu na askari wake wakabeba maiti yake hadi Bagamoyo na kuikabidhi kwa wamisionari nao; wakaridi nyumbani. Kifumigulu alipofika nyumbani alikuta mikutano haifanyiki tena kwa kuwa yeye ndiye aliyekuwa mwenye kiti. Baada ya muda mfupi tu naye Mtemi akapatwa na ugonjwa wa malale, uliomuua Bwana Stoxes na kufa. Mahali pake pakachukuliwa na mdogo wake Ndwikwa Kapela II, akawa ndiye Mtemi.

Wakati huo Wajeremani walishaanza kuitawala Tanganyika - walikwenda kujenga mnara wa ukumbusho katika kaburi la Mtemi Mirambo. Watemi ambao walikuwa ni adui wa Mirambo walienda kulibomoa kwa sababu hawakupenda kuwa na kumbukumbu na habari za Mirambo. Hakuna habari zinazoeleza kuwa Wajeremani walichukua hatua gani baada ya kubomoa kaburi hilo.

Maelezo ya habari hizi yametolewa na:

1 . Mtemi Ndwikwa Kapela II (ambaye yupo kwa sasa)
2 . Msananga aliyekuwa anabeba bendera ya Mtemi Kapela, ndiye aliempa maelezo Ndwikwa.
3 . Mpemba Gandi ambaye alikuwa askari wa Kapela.
4 . Ndasa ya Mhulu II ambaye babu yake alipigana na Mirambo.
5 . Itimba Mayunga.
6 . Magushi mama yake alishuhudia vita vya Mirambo na Kapela.
7 . Bunolo Nyamlala aliyeonyesha Iwe Lya Shinga.
8 Magushi, Mwanangwa wa Nyamilangano.
9 . Shiwilwa Kimumu, Mwanangwa wa Lugela.
10 Shingolao Kimweli, Mwanangwa wa Kundikili.
11 . Mwalimu wa shule ya msingi Edward S.M. Magasa, aliyekusanya habari hizi.
12 . Frater Deogratias Kanijo (pastoral year 1992 –93) msahihishaji na mpiga chapa.

Wakati huu Padre Georges Paquet alikuwa Paroko wa nchi zote Ukune mpaka Bulungwa.

Mtemi Ndwikwa Kapela.

Mtemi George Ndwikwa ,waswezi na ngoma zake (1994)

Mtemi Ndwikwa Kapela alizaliwa mnamo tarehe 22.4.1922 katika nchi yake ya Ukune, kijiji cha Iboja.Alifanya kwanza kazi ya Bwana ndorobo. Alitawala kama Mtemi mwaka 1952 mpaka tarehe 2.10.1962. Baada ya utemi, aliteuliwa kuwa Katibu Tarafa (Tarafa ya Msalala) Aliendelea kufanya kazi hadi alijiudhuru mwenyewe. Aliporudi nyumbani, alifika Ikulu Igalula na Kisuke; baadaye aliamua kukaa Kisuke tu kwa sababu ya upendo kwa watu wake. Alichaguliwa kuwa Mwenye Kiti wa kijiji cha Kisuke na Mwenye kiti wa kamati ya maendeleo W.D.C. Ukune; aliendesha kipindi kimoja (miaka 5)
Kutoka Askofu Mateo Shija (Kahama) tarehe 17.10.1988 nilipewa barua niwe Paroko wa Iboja (na baadaye Ushetu pia) kuanza tarehe 28.10.1988.
Mara kwa mara, nilienda kuongea na Mtemi Ndwikwa; alinieleza mambo mengi ya maisha ya zamani, hasa juu ya P. Simeon Lourdel: Tulienda pamoja mpaka Iwe Lya Shinga na alinionyesha sehemu ya nyumba ya Mapadre. Tarehe 27.1.1991, P. John heigl alimbatiza Mtemi katika kigango cha Kisuke kwa jina la Georges (joji). Wakati wa sikukuu mbali mbali alikuwa anavaa nguo zake za utemi kanisani Iboja na ni yeye alikuwa anawapa bendera kwa watu wa ngoma yangu.
Alikufa tarehe 13.10.2004, saa 10 jioni.

Mtoto wake Paulo Nkinga Ndwikwa, aliyezaliwa tarehe 2.3.1953 na kubatizwa tarehe 17.8.1963: alichaguliwa kuwa Mwenye Kiti wa Iboja tangu 1982 mpaka 1994 , na baadaye alichaguliwa kuwa Diwani wa Kata Ukune mpaka leo.
Aliteuliwa na baba yake kukaa hapo Ikulu ya zamani na kutunza na kulinda makaburi ya Watemi; pia viti vya utawala na ngoma za jadi, mikuki yote na vifaa vyote vya utawala alikabidhiwa kuvilinda na kuvitunza.

Georges Paquet, wa kabila ya Segusiav, Ufaransa.

Usongo 1980

Bulungwa (1995) mtemi Daudi

Retour